

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



HATIMAYE BENKI YA DUNIA YAFUNGUA MILANGO KWA KILA MTU

Leo hii Benki ya Dunia imetangaza kufungua milango katika taarifa zake inazozihifadhi kitakwimu ili jamii yote iweze kuziona na kuzitumia katika kusaidia watu masikini na nchi masikini zisizo na uwezo.

“Benki hiyo ya Dunia imegundua kuwa uwazi na kuwajibika ni vitu muhimu sana katika maendeleo ndio maana sasa Benki ya Dunia inatoa taarifa zao bure , wazi na kwa njia rahisi kwa watumiaji wote wanaoishi katika ulimwengu wenye viashiria vya maendeleo visivyopungua 2000 ukijumlisha na vile mia moja vya miaka 50 iliyopita.” alisema Rais wa Benki ya Dunia, Bw. Robert B. Zoellick.

Taarifa hizo zitapatikana kwa lugha ya kiarabu, Kifaransa na kiispania pamoja na kiingereza.

“Ni muhimu kwa kila mtu kuwa na taarifa na ufahamu wa mambo yanayofanywa na Benki ya Dunia,” alisema Bw .Zoellick. “Takwimu zinaeleza historia ya maendeleo ya watu na nchi kwa ujumla wake na zinaweza kusaidia sana katika kuondoa umasikini na kuongeza kuwa taarifa hizo zinapatikana kiurahisi katika mtandao kwa watumiaji wote, na vilevile zinaweza kutumika katika kuleta maendeleo. ” Alisisitiza Bw. Zoellick.

Banki ya Dunia imefanya kazi kwa umakini wa hali ya juu katika kupata takwimu hizo, imeshirikiana na washirika wa takwimu katika kupata na kuweka taarifa hizo. Kwa kufanya hivyo wameweza

kuunda **“worldbank.org,”** ambayo ni njia rahisi kwa watumiaji wa taarifa katika mtandao husika. Alisisitiza Raisi huyo.

Miezi michache ijayo Benki ya Dunia itazindua **“Apps for Development”** hii itasaidia katika kuleta ushindani wa kimaendeleo na kukabiliana na changamoto katika kuleta maendeleo kwenye jamii. Benki ya Dunia imekuwa na lengo la kuweka zana imara ili watu waweze kujiletea maendeleo.

Ufunguzi huu wa taarifa utaenda sambamba na uzinduzi wa viashiria vya maendeleo Duniani (World Development Indicators)- WDI 2010, pamoja na kufungua milango katika viashiria hivyo Duniani vyenye kufikia 1000. Juhudi zimefikwa kwenye maendeleo ya kifedha Duniani kote, kwenye viashiria vya maendeleo Afrika, kwenye ufuatiliaji wa kiuchumi Duniani na kwenye viashiria vinavyotokana na taarifa za biashara.

Upatikanaji wa taarifa hizi utawawezesha watunga sera, watafiti na hata wanajamii kufuatilia jinsi sera zinavyofanya kazi, kuleta mafanikio na kupima maendeleo kwa umakini zaidi. Alisema Bw. Zoelleck.

Benki ya Dunia itaendelea kutoa taarifa hizi katika miezi ijayo na watumiaji wanashauriwa kutoa maoni yao na kutumia taarifa hizo ipasavyo.

Ushirikishwaji wa utumiaji wa takwimu hizi utafuatiwa na uzinduzi wa urahisi wa upatikanaji wa habari za kisera wa Benki ya Dunia hapo July 2010 ambao utafanya kuwe na upatikanaji wa taarifa sahihi na za wakati.

Aidha katika taarifa iliyosomwa leo na Bw. Justin Yifu Lin, ambaye ni Chifu wa Uchumi na Makamu Mwandamizi wa Maendeleo Kiuchumi amesema kuwa kuweka hizi taarifa wazi na bure kwa watu wote ni kukamilika kwa ndoto yao. Aliendelea kueleza kuwa, mwaka huu WDI itaelemea zaidi katika malengo ya millennia (MDG). Aliendelea kuwa katika miaka kumi sasa maendeleo yameonekana katika

kufikia lengo lililowekwa.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa leo, Bi Shaida Badiie ambaye ni Mkurugenzi wa kundi linalo kusanya taarifa za maendeleo na kuzalisha viashiria vya maendeleo Duniani, alisema kuwa, "Kitu muhimu katika kupambana na umasikini ni kuimarisha mfumo wa takwimu katika nchi masikini. Serikali, wananchi, mashirika ya misaada yanahitaji takwimu ili kutengeneza sera zao."

**Imetolewa na Msemaji Mkuu
Wizara ya Fedha na Uchumi
Washington DC
20/04/2010**